JANGLE GREEN

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA**

**Shule Ya Sekondari Izazi**
**S.L.P.590 Iringa.**
**…./…/…. ..**

Namba Za Simu
**MKUU WA SHULE; Amelye J. Longo**
**0775260384/0752160384**
MAKAMU MKUU WA SHULE
**0672330064/0752916882**

**Ndugu,**

**Mzazi/Mlezi Wa**

**______________________________________________________________________________**
**_____________________________________________________________________**

**YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI **IZAZI HALMASHAURI YA** WILAYA YA **IRINGA, MKOA** WA **IRINGA** MWAKA **………..**

**1.0 UTANGULIZI**

Kwa niaba ya Jumuiya ya **IZAZI SECONDARY SCHOOL**, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na shule yetu. Kuchaguliwa kwako kumezingatia mafanikio uliyoyapata katika kuhitimu elimu ya kidato cha Nne na matokeo mazuri uliyopata katika mtihani wa Taifa. Shule hii inapokea wanafunzi mchanganyiko wa kutwa kwa kidato cha I hadi IV na bweni kwa kidato cha V na VI ambao ni **wasichana tu**. Hata hivyo zipo nafasi chache za hostel kwa kidato cha I- IV. Nafasi hizo hutolewa kwa wale tu wenye shida ya mahali pa kuishi hapa Izazi. Michepuo inayofundishwa katika shule hii kwa kidato cha tano na sita ni **CBG** na **HKL**.

Nafurahi kukuarifu Kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha **tano** katika shule hii mwaka **……….. katika tahasusi ya ______________________.**

Muhula wa masomo unaanza tarehe ……………… mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **……………** mwisho wa kuripoti ni tarehe **…………………………..**

**1.1 MAHALI SHULE ILIPO**

**SHULE YA SEKONDARI IZAZI** ipo kata ya **IZAZI** Halmashauri ya **Wilaya ya Iringa.**
Kwa kutokea **Iringa mjini**, shule ipo umbali wa **km 82** barabara ya **Iringa-Dodoma** katika kijiji cha **izazi.** Vilevile kwa upande wa kutokea **Dodoma jiji**, shule ipo umbali wa **km 172** barabara ya **Dodoma - Iringa** katika kijiji cha **izazi.**

### 1.2 Usafiri

Usafiri wa basi kutoka **Iringa** unapatikana stendi kuu ya zamani ya mabasi **Iringa-Mjini** na stendi kuu mpya ya mabasi ya **Mkoa wa Iringa** iliyopo **Igumbilo**. Nauli yake ni Tsh **5,000/-**

Usafiri wa basi kutoka **Dodoma** unapatikana stendi ya mabasi ya **Mkoa wa Dodoma** iliyopo **Nane nane**. Nauli yake ni Tsh **10,000/-** Kituo cha kushukia ni **Izazi, Kisha utachukua usafiri wa pikipiki utakaokufikisha shuleni kwa shillingi elfu mbili (2,000/=)**

**Karibu sana IZAZI SECONDARY SCHOOL, nakutakia safari njema ya kuja hapa**

## 2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

### 2.1 SARE YA SHULE

**Shule ni ya bweni na ni ya wasichana kwa A-LEVEL pekee hivyo sare ya shule ni kama ifuatavyo.**

a. Sketi mbili rangi ya **JANGLE GREEN** mshono wa rinda box **isiyo bana mwili**, **pana na ndefu inayofika kwenye kifundo cha mguu** (kitambaa kizito cha suti grade 1)

b. Shati nyeupe mbili mikono mirefu.
   - **Kwa wanafunzi watakao vaa hijabu,** juba iwe nyeupe yenye urefu wa kufika usawa wa nyonga, Nusu kanzu inayofika kwenye magoti (hijabu zote ziwe za kitambaa cheupe aina ya halua au babi. (sio kitambaa cha mpira au aina nyingine).
   - Shamba dress ni ushungi/kilemba cha rangi ya **nyeupe** kirefu kinachofunika kifua

c. Viatu vyeusi visivyo na visigino virefu, shingo ndefu wala urembo wowote vya kufunga na kamba, jozi mbili (2).

d. Soksi ndefu nyeupe. Jozi mbili.

e. Sweta moja ya mikono mirefu rangi ya **JANGLE GREEN** iliyokolezwa **shingo V**

f. **Mavazi ya michezo**.
   - T-shirt(jezi) rangi **pink (inter miami)** pamoja na bukta zake
   - Skin tight nyeusi 02 ziwe ndefu kusitiri mwili
   - Raba kwaajili ya michezo jozi 01.
   - Trak suti rangi ya **kijivu.**
   - Viatu vya mpira wa miguu kwa wachezaji

g. Nguo za kushindia (Shamba dress) sketi kitambaa **rangi ya khaki** mshono wa rinda box isiyo bana mwili, pana na ndefu inayofika kwenye kifundo cha mguu, **na** T-shirt mbili (2) za kushindia zinapatikana shuleni **(kwa shilling 30,000/= )**.

h. Nguo za nyumbani haziruhusiwi isipokuwa aje na **kanga/vitenge pair moja tu** atatumia wakati wa kuoga

### 2.2 MICHANGO YA SHULE

| NA | AINA YA MCHANGO | KIASI (Tsh) |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/- |
| 2 | Tahadhari | 5,000/- (hairudishwi) |
| 3 | Nembo | 5,000/- |
| 4 | Kitambulisho | 5,000/- |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**TANBIHI: MALIPO YOTE YAFANYIKE KUPITIA BENKI KWENYE AKAUNTI NAMBA *60510046910* - NMB YENYE JINA *IZAZI SECONDARY SCHOOL***

**(Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).**

**2.3 Mahitaji Mengine muhimu kwa matumizi binafsi ya mwanafunzi.**

a. Godoro la futi 2.5
b. Mto 1
c. Shuka za pinki 2 na foronya 2
d. Ndoo ya kuogea ya lita 10 moja.
e. Chandarua nyeupe futi 3
f. Vyombo vya chakula sahani, bakuli, kikombe, kijiko.
g. Nguo za ndani za kutosha
h. Kandambili za kuogea. (siyo yeboyebo).
i. Taulo 1, taulo za kike (Pads) si chini ya paketi 5
j. Vifaa vya masomo (taaluma)
p. Ream 02 za karatasi A.4 (kampuni ya Aone GSM).
q. Scientific calculator kwa watakao soma sayansi.
r. Fedha za kutosha za matumizi binafsi ya mwanafunzi
s. Faili (**Spring file**) dogo la kutunza kumbukumbu za mwanafunzi.
t. Ni lazima mwanafunzi akaja na **kadi ya bima ya afya au aje na tsh. 50,400**/= kwa ajili ya bima ya afya kwa matibabu ya mwaka mzima (NHIF). kadi ya bima afya itakaguliwa au pesa itapokelewa siku ya kuripoti.
u. Ni vema mzazi ukahakikisha mtoto anapokuja shuleni awe amechukua **tahadhari zote za kiafya.**
v. Trunker (sanduku la chuma).
w. Ndoo moja lita ishirini kwa matumizi ya shule.
x. Saa ya mkononi isiyo ya mshale (kwa ajili ya kutunza muda) kwa matumizi yake binafsi.

**2.4 Vitu visivyoruhusiwa shuleni.**

(a) Simu za mkononi (charger, line za simu, vocha na vyote vinavyoendan na simu) Mawasiliano muhimu baina ya mzazi/Mlezi na mwanafunzi yafanyike kupitia kwa Mkuu wa Shule kwa anuani tajwa hapo juu.
(b) Pasi za umeme, heater, birika la umem
(c) Kusuka nywele au kuweka dawa za aina yoyote ile.
(d) Kupaka rangi kucha au kupaka ina, wanja na lipstic.
(e) Nguo za nyumbani zisizo sare ya shule.
(f) Heleni, Mkufu, pete na bangili.

**3.0: Sheria na Kanuni muhimu za shule.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, sayansi, teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu chini ya ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleini.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni na asubuhi (preparation)
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shuleni na nyingine utakazopewa
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa wanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
(i) Kutunza mali za umma
(j) Mwanafunzi anatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote awapo shuleni.

**3.1: Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha KUFUKUZWA** au **KUSIMAMISHWA** shule

(a) Wizi.
(b) Utoro
(c) Uasherati na ushoga.
(d) Ubakaji.
(e) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
(f) Kupigana na kupiga.
(g) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
(h) Kudharau Bendera ya Taifa.
(i) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
(j) Kutoa mimba.
(k) Kuoa au kuolewa.
(l) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu.
(m) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(n) Kuwa na simu ya mkononi.

**4.0: Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wakutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**5.0:** Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Mwisho kabisa nachukua nafasi hii tena kukukaribisha sana hapa Izazi Sekondari na ni matarajio yangu kuwa ufikapo hapa utaitumia vema fursa hii muhimu uliyotunukiwa na taifa lako kwani wengi wameikosa.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

……………………………………………..

**AMELYE JACKSON LONGO**

**MKUU WA SHULE**

**6.1: (a) MEDICAL EXAMINATION.**

**PRIME MINISTER'S OFFICE,**
**REGIONAL ADMINSTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**IRINGA DISTRICT COUNCIL**

To the Medical Officer,

______________________________

______________________________

**REF: - REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**OF________________________________________________________ STUDENT**

Age ______________________________________________

1. Blood count (red and white)____________________________________________________________
2. Urine examination
3. Stool examination ____________________________________________________________
4. Syphilis __________________________________________________________________________
5. T. B Test ________________________________________________________________________
6. Ear Test__________________________________________________________________________
7. Eye Test__________________________________________________________________________
8. Spleen ___________________________________________________________________________
9. Abdomen _________________________________________________________________________
10. Urine for pregnant_____________________________________________________________
11. Additional information or any other physical, mental, hereditary of infectious diseases

_______________________________________________________________________________________

Treatment after examination

_______________________________________________________________________________________

**MEDICAL CERTIFICATE**

I certify that the above concerned has been examined and found **fit/not fit*** to pursue for further education.

Signature___________

Designation__________

Station ___________________

Date________________________

(Official stamp)

**Fomu hii ijazwe kikamilifu na daktari na mwanafunzi aje nayo siku ya kuripoti shuleni**

(sehemu ya kwanza ya fomu hii ijazwe na mwanafunzi na sehemu ya pili ijazwe na mzazi ua mlezi)

| **Picha** |
|---|

## SEHEMU YA KWANZA

(sehemu hii ijazwe na nwanafunzi mwenyewe)

Mimi ____________________ (mwanafunzi) kwa hiari yangu nakubali nafasi naahidi kutoshiriki/kuanzisha migomo, fujo na makosa ya jinai na nitafuata sheria zote za shule.

Jina la mwanafunzi_________________________________________

Sahihi ya mwanafunzi__________________

Tareh________________

## SEHEMU YA PILI

(Sehemu hii ijazwe na mzazi/mlezi)

Mimi __________________________________________ Mzazi/Mlezi***** wa _________________________________

**Nakubali/ Sikubali*** nafasi aliyopewa mtoto wangu na kwamba muda wote awapo shuleni atalazimika kuwa mtii kwa walimu, wazazi, viongozi na jamii kwa ujumla. Atalazimika kufuata sheria zote za shule.

Naahidi kuwa mwanangu atazifuata taratibu zote za shule hadi atakapo maliza shule.

Jina la Mzazi/Mlezi*****_______________________________________
Sahihi __________________________

Tarehe___________________________

***Futa isiyohusika**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI IZAZI**
**TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI**

**(Fomu hii ijazwe na Mzazi/mlezi)**

1. Jina kamili la Baba/ Mama/Mlezi*______________________________
2. Mahusiano na wanafunzi (Baba/Mama/Mjomba n.k) ______________________________
3. Namba ya kitambulisho cha NIDA______________________________
4. Elimu yake ______________________________
5. Kazi yake ______________________________
6. Namba ya simu ______________________________
7. Anuani______________________________ Mji/mkoa ______________________________
8. Barua pepe ______________________________
9. Mahali anapoishi Mtaa/Kijiji ______________________________Kata ______________________________

   Wilaya ______________________________ Mkoa______________________________

10. Wazazi wanaishipamoja? NDIYO ☐ HAPANA ☐

11. Mtoto anaishi na BABA MLEZI? NDIYO ☐ HAPANA ☐

12. Wazazi wote ni wazima? NDIYO ☐ HAPANA ☐

    Kama Hapana, mzazi yupi amefariki? ______________________________
13. Tarehe ya kuzaliwa ya mwanafunzi ______________________________
14. Namba ya cheti cha kuzaliwa ______________________________
15. Dini ya mzazi/mlezi*______________________________
16. Dhehebu ______________________________

17. Anuani kamili ya sehemu ambako mtoto atakuwa anakwenda wakati wa likizo kama ni nje ya eneo ambalo mzazi/mlezi anakaa ______________________________

18. Mimi ______________________________Mzazi/Mlezi* wa ______________________________nakiri kuwa taarifa nilizozitoa hapo juu ni sahihi.

    Naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi, na mwenye bidii.

    **NB:** ***Hakikisha unaambatanisha nakala ya cheti cha kuzaliwa cha mwanafunzi na kitambulisho cha*** **NIDA cha mzazi/mlezi kama kipo**